# USAWIRI WA WALIMU KAMA MAWAKALA WA KULETA MABADILIKO KATIKA JAMII KATIKA DIWANI YA *TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE*

**KONGAMANO LA TAIFA LA WALIMU LINALOANDALIWA NA TSC**

**KICC NAIROBI**

**JUNI 14 -15 2019**

**JACKSON NDUNG'U MWANGI**

**SHULE YA UPILI YA NDURURUMO**

# SABABU YA KUCHAGUA MADA

- Mwalimu ni kiungo muhimu sana katika kuleta mabadiliko katika jamii. Hii ni kwa sababu mwalimu huwa na jukumu la kipekee la kuwapasha wanafunzi wake habari, mawazo na mafundisho ambayo kwa kawaida huweza kuleta mabadiliko anuwai katika maisha yao.
- Mabadiliko haya yanaweza kuwa chanya au hasi.
- Siku za hivi karibuni, walimu wengi nchini Kenya wamelaumiwa kuwa hawatekelezi majukumu yao ipasavyo na hivyo, kufanya kiwango cha elimu nchini Kenya kudorora.
- Isitoshe, kuna baadhi ya walimu ambao wametuhumiwa kujihusisha na matendo yasiyokuwa na nidhamu na yenye kukera sana katika jamii.
- Vile vile, mwalimu amesawiriwa kwa njia hasi na vyombo vya habari, hivyo kushusha hadhi ya mwalimu na taaluma ya ualimu kwa ujumla katika taifa.

# UTAFITI HUU ULIHUSISHA NINI??

- Licha ya kuwa mwalimu nchini Kenya amesawiriwa kwa njia hasi, Utafiti huu ulinuia kuchanganua nafasi na mchango wa mwalimu wa kisasa katika kuleta mabadiliko chanya katika jamii.
- Utafiti huu ulijikita katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* iliyohaririwa na Alifa Chokocho na Dumu Kayanda (2016). Mtafiti alinuia kuihakiki diwani hii kwa vile ndicho kitabu cha lazima cha hadithi fupi kilichoteuliwa na kuidhinishwa na KICD kusomwa na wanafunzi wote wa shule za upili nchini Kenya. Vile vile, licha ya kuwa diwani yenyewe imeshughulikia masuala mengi ibuka na yenye uketo katika jamii, hadithi ya *Mwalimu Mstaafu* imemsawiri mwalimu wa kisasa kwa njia mbalimbali.

# MADHUMUNI MAKUU

- Madhumuni makuu yalikuwa ni kutathmini mchango wa walimu kama mawakala wa kuleta mabadiliko katika jamii kwa kurejelea hadithi ya *Mwalimu Mstaafu* inayopatikana katika diwani ya *Tumbo Lisiloshiba na hadithi Nyingine*

# MWEGA WA NADHARIA

Utafiti huu uliongozwa na **nadharia ya uyakinifu wa kijamii.** nadharia ya uyakinifu wa kijamii ambayo iliasisiwa na Stalin mwaka wa 1934, miaka michache baada ya mapinduzi ya Urusi ya mwaka wa 1917.Nadharia hii inaeleza kuwa uyakinifu wa kijamii una uwezo wa kusawiri jamii katika ukamilifu wake na kuonyesha hatua za jamii hiyo za kimabadiliko.

**MIHIMILI YA NADHARIA YA UYAKINIFU WA KIJAMII.**

Nadharia ya uyakinifu wa kijamii huongozwa na mihimili ifuatayo:

1. Nadharia hii husawiri jamii katika ukamilifu wake na kuonyesha hatua za jamii kimaendeleo. Huwa na wahusika wa kimaendeleo ambao hunuia kupindua na kuibadilisha hali yao ya maisha.
2. Wahusika hutekeleza matendo yao kitabaka pamoja na kusawiri matukio kihistoria. Hufanya hivi kimakusudi au bila kufahamu.
3. Uyakinifu wa kijamii huzingatia hali halisi ya jamii, Hushughulikia na kuyasawiri masuala halisi yanayotendeka katika jamii na ulimwengu wa kawaida kwa jumla.
4. Wahusika huonyeshwa kiuyakinifu.
5. Huonyesha matumaini juu ya kizazi cha binadamu.

# MUUNDO WA UTAFITI

- Utafiti huu ni wa kiuthamano na kimaelezo na ulifuata muundo wa uchanganuzi wa makala ambapo maelezo yetu yaliangazia masuala yanayohusu nafasi na mchango wa mwa walimu kama mawakala wa kuleta mabadiliko chanya katika jamii. Makala ya kimsingi ya utafiti huu yalikuwa kusoma hadithi fupi iitwayo **Mwalimu Mustaafu** inayopatikana katika Diwani ya **Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine** ilhali makala ya sekondari yalitokana na usomaji wa vitabu na makala mbalimbali yaliyohusu mada na nadharia.

# UTEUZI WA SAMPULI

- Utafiti huu ulijikita katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* iliyohaririwa na Alifa Chokocho na Dumu Kayanda (2016).
- Mtafiti alinuia kuihakiki diwani hii kwa vile ndicho kitabu cha lazima cha hadithi fupi kilichoteuliwa na kuidhinishwa na KICD kusomwa na wanafunzi wote wa shule za upili nchini Kenya.
- Vile vile, licha ya kuwa diwani yenyewe imeshughulikia masuala mengi ibuka na yenye uketo katika jamii, hadithi ya *Mwalimu Mstaafu* imemsawiri mwalimu wa kisasa kwa njia mbalimbali.
- Mtafiti aliteua diwani hii kimaksudi kwani ndiyo ingempa habari na data aliyohitaji

# DHANA KUHUSU WALIMU NA MTAZAMO HASI KATIKA JAMII

- Kwa mujibu wa Mwangi (2017) mwalimu ni mtu anayewasaidia watu wengine kupata ujuzi, maarifa na tunu. Anaendelea kudai kuwa majukumu ya mwalimu yanaweza kutofautiana kadri na jinsi anavyotangamana na utamaduni husika.
- Kwa mujibu wa makala ya Taasisi ya Elimu Tanzania (2016) imebainika kuwa ijapokuwa mwalimu katika jamii huwa na majukumu ya kipekee, yeye hukumbana na matatizo mbalimbali pamoja na changamoto mbalimbali. Baadhi ya changamoto hizi ni kama vile kulipwa mshahara duni, kutodhaminiwa na wazazi, kufunzia katika mazingira ambayo hayafai na kukosa vifaa vya kutosha katika kufunza.
- Akizingatia kuhusu suala la kazi ya ualimu, Roy (2006) anadai kuwa Ualimu ni taaluma bora kabisa miongoni mwa taaluma zote zilizopo duniani. Ualimu ni kazi ya kuheshimika. Siku hadi siku na hatua kwa hatua, walimu huyatengeneza maisha ya wanafunzi wao. Roy anaendelea kudai kuwa katika jamii, nyingi walimu hulipwa kiasi kidogo sana cha mshahara ukilinganisha na kazi waifanyayo.

# DHANA KUHUSU WALIMU NA MITAZAMO HASI KATIKA JAMII..CONT…..

- Zachariah(2016) katika makala yake alidokeza kuwa licha ya mitazamo hasi ambayo wanajamii huwaelekezea walimu, imetambulika kuwa baadhi ya shutuma ambazo huelekezwa walimu huwa hazina mashiko. Alibaini kuwa wakati mwingi, waalimu hutekeleza majukumu yao ipasavyo ijapokuwa wanakosewa heshima na wanajamii pamoja na taasisi zingine kama vile vyombo vya habari pamoja na magazeti.
- Kwa mujibu wa makala ya CHAKITA (2012), mwalimu ni kiungo muhimu sana katika mchakato mzima wa upashanaji maarifa. Licha ya kuwa wamesawiriwa kwa mtazamo hasi katika jamii, walimu wengi katika jamii hujitolea mhanga kuhakikisha kuwa wanafunzi wao wamepita mitihani yao.
- Mapitio haya ya maandishi yanakuza msingi wa suala la utatifi lililoangaziwa katika utafiti huu. Utafiti huu unanuia kutathmini mchango wa mwalimu katika kuleta mabadiliko bora miongoni mwa wanafunzi katika jamii licha ya kuwa wanasawiriwa kwa mtazamo hasi na wajamii.

# UCHANGANUZI WA DATA

## Walimu kama mawakala na visababishi vya mabadiliko katika hadithi fupi ya *Mwalimu Mstaafu* inayopatikana katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi nyingine*

- Mabadiliko katika jamii yanaweza kuwa ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.
- Mwalimu katika jamii huwa na jukumu la kipekee katika kukuza maadili na kupasha habari muhimu kwa wanafunzi wake.
- Isitoshe, mwalimu huwa ni chemichemi na bubujiko la maarifa yenye manufaa mengi kwa wanajamii. Nchini Kenya, mwalimu huwa na jukumu la kipekee la kufanikisha maazimio na sera za kiserikali kama vile kuleta utangamano katika jamii.
- Licha ya haya, walimu nchini Kenya wanakabiliwa na changamoto nyingi sana kwani baadhi ya wananchi wanawasawiri kwa mtazamo hasi na kuwaona kama watu wasio na manufaa yoyote katika jamii.
- Wanasawiriwa kuwa wazembe, wabinafsi na waliopotokwa na maadili. Kwa mujibu wa utafiti huu, mtafiti aliangazia jinsi mwalimu anavyotekeleza nafasi muhimu katika kuleta mabadiliko mazuri kwa kurejelea hadithi ya ***Mwalimu Mstaafu*** inayopatikana katika diwani ya ***Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine***.

# UCHANGANUZI CONT…

**1 Jukumu la mwalimu kuwafinyanga na kuwapata wanafunzi taaluma katika jamii**

- Kwa mujibu wa hadithi hii ya *Mwalimu Mstaafu*, kuna mwalimu aliyependeka sana aliyeitwa Mwalimu Mstaafu.Tunaelezwa kuwa aliyabadilisha maisha ya wanafunzi wengi waliopitia mikononi mwake kutokana na jinsi alivyowafunza kwa umakinifu na kujitolea. Inabainika kuwa mwalimu huyu licha ya kuwa alikuwa akiistaafu, aliwafinyanga wanafunzi wake barabara na kuwafanya wawe madaktari, marubani, wabunge, mawaziri, wahandishi na kadhalika kutokana na juhudi zake za kipekee kama inavyobainika katika ukurasa wa 120.

*"Mwalimu Mstaafu ambaye Mikononi mwake, wanafunzi wengi walifinyangwa barabara mpaka hatimaye wakaishia kuwa madaktari, marubani, wabunge, mawaziri, wahandishi, wahasibu…"*

- Mfano huu unadhihirisha jukumu la kipekee la Mwalimu huyu ambaye kupitia kwake, aliweza kuyabadili maisha ya wanafunzi wengi na kuwafanya watu tajika na wenye taaluma za kupendeka katika jamii. Jukumu lake Mwalimu Mtaafu linachangia zana katika kuleta mabadiliko chanya miongoni mwa wanajamii katika jamii hii. Anafanikiwa kuhakikisha kuwa amewapasha wanafunzi hawa maarifa ya kipekee yenye kuwafanya kupendeka na kudhaminiwa katika jamii.

# UCHANGANUZI CONT…

## 2. Mwalimu kuwapa wanafunzi ushauri nasaha maishani

- Licha ya kuwa Mwalimu huyu alikuwa anawapasha wanafunzi wake maarifa anuwai na yenye umuhimu katika jamii, tunaelezwa kuwa alitekeleza jukumu lingine la kipekee la kuwapa wanafunzi wake ushauri nasaha. Ushauri huu uliwasaidia wanafunzi kupata maarifa na ujuzi wa kuweza kuishi na kutangamana na wenzao kwa njia nzuri na yenye kuleta amani na maelewano. Ushauri huu pia humsaidia mwanafunzi kufanya maamuzi yafaayo katika jamii na kuishi katika maisha yenye kupendeka na kudhaminiwa.
- *Wanafunzi wake wote hao, wanafunzi wake hawamsahau kwa nasaha zake, kwa insafu yake, kwa hurumza zake, kwa hekima yake, kwa ustaarabu wake, kwa uadilifu wake, kwa uwajibikaji wake, kwa nemsi yake, kwa ucheshi wake, kwa ukaramshi wake- kwa yote na yote. Ukurasa wa 120*.
- Kupitia hali hii ya kuwapa wanafunzi wake ushauri nasaha, wanafunzi wake waliishia kumpenda na kumdhamini sana. Isitoshe, aliwasaidia sana katika kukuza maadili yao na hivyo kuwafanya watu wenye kufanikiwa na kutegemewa katika jamii. Mfano huu unadhihirisha kuwa licha ya mwalimu nchini Kenya kulaumiwa kutotekeleza wajibu wao ipasavyo, Mwalimu Mstaafu ni kielelezo kizuri cha mwalimu mwenye kujituma katika kazi yake na kuwashauri wanafunzi wake kwa njia ipasayo.

# UCHANGANUZI CONT…

**3 Mwalimu kubadili maisha ya wanafunzi wake kwa kutumia nyenzo na mbinu anuwai**

- Ili kupitisha maarifa, maadili pamoja na ushauri nasaha kwa wanajamii, Mwalimu Mtaafu anaonekana akitumia mbinu anuwai za kufundishia ili wanafunzi wake waweze kufanikiwa na kuwa watu wenye kuleta mabadiliko katika jamii.
- Ili mwalimu aweze kufanikisha somo lake darasani, ni sharti aweze kutumia mbinu na nyenzo mbali mbali za kufunza ili somo lake liweze kueleweka na kudhaminiwa na wanafunzi.
- Kama kielelezo cha mwalimu bora na mwenye kuwajali wanafunzi wake, Mwalimu Mstaafu anatekeleza masomo yake kwa njia yenye kufana na iliyo bora zaidi. Kwa mujibu wa hadithi hii, tunaelezwa kuwa alikuwa mcheshi sana na mkakamavu, jambo lililomfanya apendwe sana na wanafunzi wake.
- Isitoshe, alikuwa muadilifu na mwenye mfano mwema, hali iliyomfanya apendeke na adhaminiwe na wanafunzi wake. Tafiti mbalimbali zimeonyesha kuwa uwezo wa mwanafunzi kuelewa somo la mwalimu hutegemea mambo mengi kumhusu mwalimu mwenyewe. Mwanafunzi huwa makini kuchunguza mbinu na nyenzo alizozitumia mwalimu na uadilifu wa mwalimu husika. Sifa hii ya Mwalimu Mstaafu iliweza kuwavutia sana wanafunzi wake na kuwafanya kumsikiza kwa umakinifu. Isitoshe, tunaelezwa kuwa alikuwa mwalimu aliyejawa na hekima, mwenye huruma na aliyewajibika katika kufunza soma lake.

# UCHANGANUZI CONT…

**4.Mwalimu kuwa na subira na umakinifu ili aafikie lengo lake**

- Akiwa Mwalimu wa shule ya msingi na chekechea. Mwalimu Mtaafu alitekeleza jukumu la kipekee katika kuwafunza na kubadili maisha ya wanafunzi wake wakiwa katika umri wa chini.
- Tunaambiwa kuwa mwalimu kwa huruma na kuwajibika kwake, hakusita

*“ Kuwashikisha kalamu, kuwafichulia siri ya tarakimu, abjadi, ramani, michoro, jedwali, Hisabati, Sayansi, Historia na Jiografia- na vyote na vyote.”*

- Mfano huu unaonyesha jukumu la kipekee alilokuwa nalo Mwalimu huyu katika kufinyanga na kuyabadili maisha ya wanafunzi wachanga aliopewa jukumu la kuwatunza.
- Haonekani kulalamika kama wafanyavyo walimu wengine ila anajitolea mhanga kubadili maisha yao. Anachukua jukumu la kipekee na kuwaelekeza wanafunzi hawa wa chekechea kwa umakinifu wa hali ya juu.
- Bila kulalamika, anaonekana akiwafunza na kuwapa watoto hawa maarifa ya kwanza maishani mwao. Kutokana na mfano huu. Ni bayana kuwa mwalimu huyu anatekeleza jukumu la kipekee la kuleta mabadiliko kwa watoto wadogo ambayo baada ya kupata maarifa yale, wanaishia kuwa watu wa kutegemewa katika jamii.

# UCHANGANUZI CONT..

**5 Mwalimu kuendeleza jukumu la kupunguza mipaka ya utabaka na ubaguzi katika jamii**

- Katika kuendeleza jukumu la kupunguza utabaka katika jamii na kuendeleza utangamano miongoni mwa wananchi, Mwalimu Mtaafu anaonekana akitekeleza jambo hili kwa kikamilifu. Hata kama wengi wa waliohudhuria kwenye karamu ile ya kustaafu kwake walikuwa matajiri, anaonekana pia akiwatambua wale ambao hawakuhitimu katika masomo na kuwapa nafasi ya kujieleza katika mkutano ule. Katika ukurasa wa 121, anasema,
- *"Mimi sikuwafundisha ubaguzi, kwa nini mnabagua? Kwa nini hamkuwapa watu wa matabaka yote nafasi ya kuzungumza? Kwa nini? Kwa nini mnafanya hali hii ya kuwa kuna watu na nusu watu? Naomba radhi mfawidhi wa sherehe lakini nadhani ni jambo la busara kutokitia mchanga kitumbua cha sherehe hii kwa kubagua. Kwa hivyo, naomba wazungumze pia wake ambao hawakuja hapa na magari mazito. Naomba wazungumzwe wale ambao hawatasifu tu."* Ukurasa wa 121.

# UCHANGANUZI CONT……..

- Mfano huu unaonyesha kuwa kwa kweli, mwalimu huyu alikuwa radhi kuleta mabadiliko katika jamii. Anajaribu kuziba mipaka ya kitabaka katika jamii kwa kuwapa nafasi wanafunzi wake wote hata wale ambao hawakuhitimu katika masomo kujieleza na kutoa maoni yao. Isitoshe, anakubali kukosolewa mabaya aliyoyatenda alipokuwa mwalimu bila kujiwekea kinyongo.
- Jairo ambaye hakuhitimu katika masomo anapata nafasi ya kumkosoa mwalimu wake. Hata anapokosolewa, haonekani kuudhika wala kukereka ila anaonyesha stahamala na kuitikia makosa yake.
- Kwa mujibu wa utafiti huu, ni bayana kuwa walimu katika jamii hii wanatekeleza majukumu ya kipekee katika kuleta mabadiliko katika jamii.
- Licha ya tuhuma ambazo walimu wengi hupata katika jamii, Mwalimu Mstaafu ni kielelezo cha mwalimu bora anayepaswa kupigiwa mfano na kuigwa na wengi.

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO…

- Kwa mujibu wa utafiti huu, ni bayana kuwa walimu wanaweza kuwa mawakala wa kuleta mabadiliko katika jamii kutokana na matendo yao mema na juhudi zao za kila siku za kuwapasha wanafunzi wao maarifa.
- Nchini Kenya kwa muda mrefu, taaluma ya ualimu imeonekana ikishushwa hadhi na kukosa kudhaminiwa.
- Isitoshe, walimu wameonekana wakidhalilishwa na kukosewa heshima katika jamii. Wamekuwa wakituhumiwa kuwa hawatekelezi majukumu yao kwa njia inayofaa. Vyombo vya habari wakati mwingine hutilia chuku masuala yanayohusiana na mwalimu na kuyasawiri kwa njia isiyofaa. Mwalimu mmoja akifanya kosa ama akiteleza katika majukumu yake, tendo hilo la mwalimu mmoja huhusishwa na kujumuishwa na walimu wote katika taifa letu, jambo ambalo halifai kabisa katika jamii.
- Ili kujaribu kuubadili mtazamo huu hasi ambayo huwafika walimu wengi nchini Kenya, utafiti huu umebaini wazi kuwa hata kama kuna baadhi ya walimu ambayo kwa njia moja au nyingine huteleza katika majukumu yao, mwalimu hutekeleza jukumu la kipekee katika kubadili maisha ya wanafunzi katika wanajamii na kuwafanya watu wa kutegemewa.

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO…

- Hadithi fupi ya *Mwalimu Mtaafu* inayopatikana katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* ni kielezo kizuri cha jinsi walimu wanavyotumiwa kama mawakala wa kuleta mabadiliko katika jamii.
- Kwa mujibu wa hadithi hii, imebainika kuwa walimu wanawafinyanga na kuwapa wanafunzi taaluma zenye kuwafaa katika jamii. Isitoshe, mwalimu anawapa wanafunzi wake ushauri nasaha maishani unaowasaidia kukabili matatizo ya kila siku katika jamii, anatumia mbinu na nyenzo mbalimbali ili kubadili maisha ya wanafunzi wake na kuwa kielelezo na mfano mwema wa kuigiwa katika jamii. Vile vile, mwalimu anaendeleza jukumu la kupunguza mipaka ya utabaka na ubaguzi katika jamii, jambo ambalo linafaa kuigwa na kutiliwa mkazo na walimu wa sasa nchini Kenya.
- Ni bayana kuwa licha ya mtazamo hasi ambao walimu wamekuwa wakisawiriwa nao, walimu ni mawakala wa kuleta mabadiliko katika jamii. Mtafiti anapendekeza tafiti zijazo zihakiki juhudi ambazo jamii na serikali kwa jumla inazoweza kuchukua ili kuimarisha hali ya mwalimu katika kuwasilisha somo lake darasani.

……….MWISHO…………

ASANTE